Imetolewa tarehe: 26 Agosti, 2010

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATOKEO YA OPERESHENI MAMBA AWAMU YA TATU ITAKAYOTOLEWA NA MKURUGENZI WA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI KAMISHNA WA POLISI ROBERT MANUMBA KATIKA UKUMBI WA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA TAREHE 26 AGOSTI 2010

Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Bwana Hiiti B. Sillo

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi Jamii,

Mkuu wa INTERPOL, Tanzania, Kamishna Msaidizi wa Polisi Bw Hussein Laisseri

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Idara ya Usalama wa Taifa,

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani (FCC),

Mwakilishi wa Kamishna wa Ushuru na Forodha (TRA),

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa,

Wanahabari,

Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wote kwa kuitikia wito wa kuja kupokea taarifa kwa umma kuhusu matokeo ya Operesheni Mamba awamu ya tatu.

Kama ilivyoelezwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TFDA, Operesheni hii ya pamoja ilifanyika kwa ushirikiano baina ya Mamlaka ya Chakula na Dawa, Jeshi la Polisi, Shirikisho la Polisi la Kimataifa (Interpol), , TAMISEMI, Tume ya Ushindani (FCC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Kitengo cha Huduma za Dawa cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Aidha, napenda kuwataarifu kuwa Operesheni hii ilifanyika sanjari katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika tarehe tofauti za mwezi Julai, 2010 kwa kuzingatia makubaliano ya pamoja yaliyofikiwa kwenye mkutano wa maandalizi uliofanyika tarehe 27-28 Aprili 2010 huko Bujumbura, Burundi kwa lengo la kufanikisha Operesheni hii kwa nchi za Afrika Mashariki.

Kwa upande wa Tanzania, Operesheni ilifanyika Tanzania Bara na visiwani. Nchi za Burundi na Rwanda pamoja na Zanzibar zimeshirikishwa kwa mara ya kwanza katika Operesheni hii. Ushirikishwaji wa nchi zote zilizopo katika Jumuia ya Afrika Mashariki ni kutokana na ukweli kuwa **biashara ya dawa bandia ni biashara haramu inayovuka mipaka (cross-boarder crime)** na hivyo inahitaji kukabiliana nayo kwa kushirikiana na nchi tunazopakana nazo.

Ndugu wanahabari,

Napenda kuwataarifu pia kuwa, chanzo cha Operesheni hii kinatokana na hali halisi ya dunia kukabiliwa na tatizo la dawa bandia ikiwa ni pamoja na nchi za Afrika Mashariki. Kutokana na hali hiyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia kikosi kazi cha kupambana na dawa bandia kiitwacho “International Medical Products Anti-Counterfeit Task Force – IMPACT” kwa kushirikiana na Shirikisho la Polisi wa Kimataifa (INTERPOL) limeonyesha nia ya

kushikiriana na nchi husika katika kupambana na tatizo la dawa bandia kwa kuendesha Operesheni.

Hivyo, Operesheni hii ni mwendelezo wa Operesheni Mamba ya pili iliyofanyika katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania mwezi Agosti 2009. Maeneo yaliyohusika katika Operesheni hii ni wilaya zote za jiji la Dar es Salaam, Arusha mjini, Namanga, Mbeya mjini, Tunduma, Shinyanga mjini, Kahama, Mwanza mjini, Geita na Dodoma mjini.

Ndugu wanahabari,

Jumla ya maeneo 225 yalikaguliwa kama ifuatavyo; Famasi 138, Maghala ya kutunzia dawa 5, Maduka ya dawa baridi/muhimu 47, Hospitali/zahanati 5 na maeneo mengine 30, Maduka ya Vipodozi 18, Mabasi ya abiria 6, Treni ya abiria 1 (TAZARA), Maduka yanayouza dawa za kichina 2, nyumba za kuishi 10 na sehemu 4 za mipaka ya nchi na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo;

	Idadi ya sehemu zilizokaguliwa					
	Famasi	**Maghala ya dawa**	**Duka la DLDB/DLDM**	**Hospitali/zahanati**	**Maeneo mengine**	**Jumla**
Dar es Salaam	114	4	16	1	3	138
Mbeya	2	-	11	3	2	18
Arusha	2	-	-	-	8	10
Mwanza	7	1	12	-	-	20
Shinyanga	3	-	5	-	3	11
Dodoma	10	-	3	1	14	28
	138	**5**	**47**	**5**	**30**	**225**

Dawa zilizokamatwa

Jumla ya aina 196 za dawa zenye thamani ya **TZS 18,308,470/-** zilikamatwa kama ifuatavyo;

Na.	Kundi la dawa	Idadi ya aina	Thamani (TZS)
1	Dawa zilizoisha muda wa matumizi	23	804,600/-
2	Dawa za Serikali na miradi ya Serikali	9	6,962,500/-
3	Dawa zisizosajiliwa	75	4,515670/-
4	Dawa moto kutoka maduka ya dawa baridi	72	3,855,700/-
5	Dawa zenye viwango duni vya ubora	6	200,500/-
6	Dawa za kutangazia biashara kwa madaktari (Physician samples)	11	1,969,500/-

Kwa matokeo haya ni wazi kuwa katika zoezi hili hakuna dawa bandia iliyokamatwa ikiashiria kuimarika kwa udhibiti wa dawa hapa nchini.

Aidha, jumla ya aina mbalimbali 6 za vipodozi vilivyopigwa marufuku vyenye thamani ya Shilingi 444,600/- vimekamatwa, ikiwa ni pamoja na aina 4 za kemikali vinavyosadikiwa kubadilisha au kuongeza maumbile ya binadamu. Vipodozi hivyo vinne ni ***Ivan Mwali Soap, Herbal skin doctor, hip up cream na Ardiour sex enhancing medicines.***

Ndugu wanahabari,

Kutokana na matokeo ya Operesheni hii, hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ambapo jumla ya majalada 40 ya kesi yamefunguliwa katika vituo mbalimbali vya polisi dhidi ya watuhumiwa. Mchanganuo wa kesi hizo katika kila mkoa ni kama ifuatavyo:-

S/n	Mkoa	Idadi ya kesi
1	Dodoma	15
2	Mbeya,	7

3	Mwanza	1
4	Shinyanga	11
5	Arusha	6
	Jumla	**40**

Aidha, baada ya uchunguzi wa makosa kukamilika hatua mbalimbali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwapeleka mahakamani watuhumiwa au kutoa adhabu kulingana na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003.

Ndugu wanahabari,

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa taasisi zilizofanikisha Operesheni hii kwa kugharamia, kushiriki kikamilifu na kutambua umuhimu wa zoezi hili kwa maslahi ya Taifa. Jeshi la Polisi linapenda kutoa wito kwa taasisi za udhibiti kuendelea kushirikiana na kuhakikisha kuwa tunapambana na tatizo la dawa bandia ili kulinda afya za watanzania.

Jeshi la Polisi limejipanga kushirikiana na taasisi **zote nchini na pia mradi wa WHO/IMPACT kwa kusaidiana na INTERPOL** katika kukabiliana na tatizo la dawa bandia nchini. Hivyo naomba nitoe wito kwa wananchi wote tushirikiane katika kukabiliana na uhalifu wa aina hii .

Pili, ninapenda kutoa wito kwa umma na wananchi kwa ujumla kuendelea kutoa taarifa za wale wote wanaojihusisha na biashara haramu za dawa bandia kwa Mamlaka au vyombo vya usalama ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Napenda kumaliza kutoa taarifa hii kwa kusisitiza kurudia ujumbe alioutoa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TFDA kuwa **"Dawa bandia ni hatari kwa afya za binadamu na husababisha vifo".**

Aksanteni kwa kunisikiliza